Ripoti ya Maendeleo ya Watu Afrika ya **2016**

Empowered lives.
Resilient nations.

Kuharakisha Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake barani Afrika



MUHTASARI

Hakimiliki © 2016
Na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
Ofisi ya Kanda ya Afrika
1 UN Plaza, New York, NY 10017, USA

Imesanifiwa na kupigwa chapa: Phoenix Design Aid, Denmark. Imechapwa katika karatasi zilizothibitishwa za FSC kwa kutumia wino unaotokana na mbogamboga.
Karatasi za chapisho hili zinaweza kutumiwa kama malighafi.

Jalada: Michoro hii ni rejea ya kidhana kuhusu ukuaji wa jamii na maendeleo ya utungaji sera. Kurudiwarudiwa kunaakisi msingi wa kimuundo na rangi zinazoelekea juu zina maana ya ukuaji kwa ajili ya maendeleo ndani ya miundodhana iliyopo. Michoro katika mavazi ya Kiafrika inawakilisha vazi la kawaida la kiasili kwa ajili ya wanaume na wanawake na ni chanzo kikuu cha shughuli za kibiashara kwa wanawake katika Bara hilo.

Ripoti ya Maendeleo ya Watu Afrika ya **2016**

Kuharakisha Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake katika Afrika

Utangulizi

Ripoti hii ya Maendeleo ya Watu Afrika ya 2016 kuhusu usawa wa jinsia inafuatia ile ya Maendeleo ya Watu Afrika ya 2012 iliyoangazia umuhimu wa kuhakikisha usalama wa chakula kwa Waafrika wote. Ripoti zote mbili zina lengo moja la kushughulikia kile kinachoonekana kuwa ni utekelezaji wa ajenda zilizokuwa bado kukamilishwa katika mwelekeo wa maendeleo ya Afrika. Yote mawili yametambuliwa kama vipaumbele muhimu kwa serikali na raia wa nchi za Kiafrika.

Ripoti ya mwaka huu kuhusu usawa wa jinsia inatathmini jitihada zinazoendelea za nchi za Kiafrika kuongeza kasi ya kuhakikisha uwezeshwaji wanawake kupitia nyanja zote za jamii – nyumbani na katika jumuiya, katika mafanikio ya afya na elimu, mahali pa kazi, na katika ushiriki wa kisiasa na uongozi. Wakati ambapo hatua kubwa zimekwishakupigwa katika maeneo mbalimbali katika nchi zilizo nyingi, usawa wa jinsia kwa wanawake na wasichana wa Afrika bado hauko katika viwango vya kuridhisha. Ili kushughulikia upungufu huu, ripoti hii inachukua njia ya uchumi jamii katika masuala ya usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake Barani Afrika.

Ujumbe mkuu wa ripoti hii ni kwamba kuweka mkazo mkubwa zaidi katika usawa wa jinsia itakuwa kichocheo muhimu na kilichochelewa sana kwa maendeleo ya watu na ukuaji uchumi wa haraka na jumuishi zaidi katika bara zima. Mkazo wa sera na programu katika kutumia vipawa vya wanawake ni msukumo muhimu wa kiuchumi na kijamii kwa maendeleo jumuishi na endelevu zaidi. Sera na programu ambazo bila kukusudia zinawaacha wanawake kando au kuwanyima haki hazitafaulu kamwe katika muda mrefu ujao. Vilevile, ukuaji jumuishi hauwezi kupatikana kama uwezeshwaji wanawake unawekwa katika vifunguvifungu, au unaonekana kama shughuli tofauti dhidi ya kile ambacho kikawaida kinaonekana kuwa ni jukumu muhimu la serikali.

Kwa maelezo rahisi, kuongeza kasi ya usawa wa jinsia ni jukumu muhimu la serikali, likihusisha jitihada za sekta mbalimbali zikiwemo taasisi za kitaifa na mahalia, watendaji wasio wa kiserikali, vyama vya kiraia na sekta binafsi. Vivyo hivyo, kushughulikia usawa wa jinsia kwa namna pana kama hiyo kunaunganisha na kuimarisha ajenda motomoto ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), ambayo serikali za Kiafrika na jamii ya kimataifa kwa pamoja wamejiwekea kwa miaka 15 ijayo. Njia pana katika kuleta usawa wa jinsia pia itaimarisha mafanikio ya Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika. Ripoti hii ya Maendeleo ya Watu Afrika ya 2016, kwa hiyo, inatoa muundo-kazi wa utekelezaji wa SGD 5 kuhusu usawa wa jinsia,

kwa namna ya pekee, na malengo mengine kwa ujumla.

Mwisho, ni muhimu kusisitiza kwamba ripoti hii imeandikwa ili kuhimiza midahalo na majadiliano kuhusu sera juu ya hatua zaidi zinazohitajika ili kuhakikisha usawa wa jinsia unaingizwa kikamilifu katika ajenda za kitaifa na majadiliano yanayoendelea ya sera kote Afrika. Ripoti imeandaliwa kwa kuzingatia walengwa tofautitofauti – watunga sera wa Afrika na watendaji, mashirika mengine ya maendeleo, sekta binafsi, vyama vya kiraia, wasomi, na raia wa Afrika vijana kwa wazee. Inatarajiwa kwamba ripoti itawashughulisha na kuchochea majadiliano na miafaka kuhusu njia mbalimbali ambazo kila nchi ya Afrika inaweza kuchukua katika kukabili changamoto zake kali za maendeleo na haki kuu za binadamu—usawa wa jinsia.

Helen Clark
Mkuu
Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa

Dibaji

Kwa niaba ya Ofisi ya Kanda ya Afrika ya UNDP, ninafurahi kuwasilisha Ripoti hii ya pili ya Maendeleo ya Watu Afrika kuhusu mada ya Kuharakisha Usawa wa Jinsia barani Afrika.

Usawa wa jinsia si kipaumbele kipya cha maendeleo kwa nchi Afrika. Kwa hakika, umuhimu wake umetambuliwa muda mrefu na Umoja wa Afrika na iliyokuwa mtangulizi wake, Umoja wa Nchi Huru za Afrika, likichukua nafasi ya juu katika kuunga mkono haki za wanawake na wasichana kwa miongo kadhaa iliyopita. Umoja wa Afrika umeuteua mwaka 2016 kama mwaka wa Uwezeshaji na Maendeleo ya Mwanamke. Hata hivyo, maendeleo katika kuleta usawa wa jinsia yamekuwa ya chini kuliko ilivyotarajiwa na yasiyo na mwelekeo thabiti kwa nchi zilizo nyingi za Afrika.

Ripoti hii kuhusu usawa wa jinsia inakusudiwa kuweka mkazo katika changamoto muhimu ya maendeleo, katika wakati ambapo Afrika imekuwa ikipitia mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kasi ya ukuaji wa uchumi katika baadhi ya nchi za Afrika miaka michache tu iliyopita ilififishwa na mtikisiko wa mahitaji ya bidhaa ghafi duniani. Machafuko ya kisiasa na kiraia kwa sababu ya kukosekana usawa, migogoro ya mahalia na matarajio yasiyofikiwa yanaendelea kuathiri nchi nyingi za Afrika. Vilevile, janga la Ebola la mwaka 2014 na ukame katika nchi za Afrika Mashariki, Magharibi na Kusini mwaka 2015/16 zinaonyesha ni kwa kiasi gani hata jamii zinazoendelea za Afrika zilivyo dhaifu na hatarini kwa majanga na mitikisiko ambayo haikutarajiwa. Katika hali hizi, wanawake wa Afrika mara nyingi hubeba kwa namna ya pekee mizigo mikubwa zaidi kama akina mama, walezi na watafutaji riziki wa kaya.

Katika uchambuzi ufuatao, ripoti inaangazia pale ambako kumekuwa na maendeleo katika kushughulikia usawa wa jinsia na wapi na mahali gani bado kuna upungufu na changamoto. Kwanza inatoa picha ya jumla kwa ufupi kuhusu maendeleo ya watu ya Afrika kwa kutumia viashiria tofauti vya maendeleo ya watu vya UNDP, kwa kuweka mkazo maalumu katika viashiria viwili ambavyo vinapima maendeleo ya jinsia na usawa wa jinsia. Zaidi ya hayo, ripoti inachambua mienendo ya jinsia na ulinganisho katika masuala ya afya, elimu, fursa za uchumi na vikwazo, nia pia uwakilishi wa kisiasa na uongozi. Mkazo pia unawekwa katika vyanzo vya msingi vya sababu kuu za kukosekana kwa kudumu kwa usawa wa jinsia, ikiwemo mila potofu za kijamii katika kupunguza kasi kuelekea katika usawa wa jinsia na mitanziko ya kisera ambayo nchi za Afrika inakabiliana nayo katika kupatanisha taratibu za kisheria na uamuzi uliopita ambao

ulikuwa na madhara kwa mila za kijamii na kimapokeo.

Ripoti pia inatathmini njia za zera na kitaasisi ambazo serikali za Afrika zimetumia ili kushughulikia ukosefu wa usawa wa jinsia na kuongeza kasi ya uwezeshaji wanawake na kuleta usawa katika fursa za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Katika ripoti nzima, ulinganisho unafanywa kati ya nchi za Kiafrika na kanda nyingine zinazoendelea, hasa Asia na Amerika ya Kusini na Visiwa vya Karibea.

Sura ya mwisho ya ripoti inatoa ajenda ya kuchukua hatua kupitia muundodhana wa sera na mkakati ambao unaweka usawa wa jinsia kuwa kiini cha ajenda ya maendeleo. 'Njia' pana nne zinapendekezwa ambazo zinatoa muundodhana wa sera na programu ili kuharakisha usawa wa jinsia na kuingiza kikamilifu suala la jinsia katika ajenda pana ya maendeleo.

Njia hizi nne zinamaanisha:

- kuunga mkono upitishwaji wa mageuzi, sera na programu ili kuendeleza uwezeshaji wanawake;

- kuunga mkono uwezo wa kitaifa wa kuhamasisha na kuongeza ushiriki na uongozi wa wanawake katika kutoa uamuzi nyumbani, katika uchumi na katika jamii;

- kuunga mkono uwezo wa kutekeleza njia mbalimbali za kisekta ili kupunguza makali ya athari za ubaguzi katika utoaji huduma za afya na elimu; na

- kuunga mkono wanawake kumiliki na kusimamia mali za kiuchumi na kimazingira.

Msingi wa njia hizi ni kwamba kwa kuhakikisha kwamba wanawake wanapata fursa sawa za kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kuhamisha kutoka sheria hadi usawa wa jinsia kamilifu ndipo serikali zinaweza kuhakikisha kwamba maendeleo yao katika ukuaji wa kiuchumi na maendeleo ya watu ni jumuishi kikamilifu kwa raia wote na endelevu kwa muda mrefu.

Tunatumaini kwamba ripoti hii itachochea mijadala na midahalo kuhusu changamoto zilizobaki na fursa ambazo hazijatumika bado kwa ajili ya hatima njema ya Afrika.

Abdoulaye Mar Dieye
Mkurugenzi wa Ofisi ya Kanda ya Afrika

Yaliyomo

Utangulizi	iv
Dibaji	vi
Mantiki ya ripoti	1
Njia ya uchambuzi	2
Upigaji hatua na changamoto katika maendeleo ya watu Afrika	4
Masuala ya kijamii kuhusu usawa wa jinsia	6
Wanawake katika uchumi wa nchi za Afrika	8
Wanawake wa Afrika katika siasa na uongozi	9
Nafasi ya sheria na mapokeo ya kijamii katika usawa wa jinsia	11
Njia za sera na programu za kushughulikia kutokuwepo kwa usawa wa jinsia	12
Ajenda ya kuchukua hatua kuharakisha usawa wa jinsia	14
Hitimisho	19
Nyongeza Faharisi ya Maendeleo ya Watu Afrika (HDI) nafasi, thamani na mienendo	20

Muhtasari

Mantiki ya ripoti

Tangu Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu miaka 68 iliyopita, Tamko la Milenia miaka 15 iliyopita hadi Malengo ya Maendeleo Endelevu leo, mkazo wa dunia umeendelea kubaki katika kuhamasisha haki za binadamu na kufuta ubaguzi na vipato visivyo vya usawa kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana. Hata hivyo, licha ya uelewa ulioenea wa haki za wanawake na manufaa yanayopatikana kwa wote katika jamii kutokana na kutendeana kwa haki na upatikanaji wa rasilimali na fursa kwa wanawake na wanaume, bado ukosefu wa usawa upo. Katika ngazi za kikanda na kitaifa, kuna kuongezeka kwa uelewa kwamba kadiri wanawake wa Kiafrika wanavyopiga hatua kubwa katika neema za kiuchumi na kijamii, kuna manufaa zaidi kwa jamii nzima, lakini licha ya kuongezeka kwa utambuzi huu, kuondoa ukosefu wa usawa kwa wanawake bado hakujafanikiwa sana. Tofauti kubwa kati ya fursa kwa wanaume na wanawake bado ni changamoto kubwa na kikwazo kizito kwa mageuzi ya kimfumo na kijamii ambayo ndiyo lengo la nchi zote za Kiafrika.

Mazingira yanayobadilika ya maendeleo – yakiwa na fursa zinazoibuka, mitikisiko na hatari—yanafanya iwe lazima kwa Afrika kuongeza kasi ya kuendeleza maendeleo endelevu na yenye usawa. Hii inaweza kupatikana kwa kujenga uwezo wa kujinusuru wa kiuchumi, kijamii na kimazingira kwa ajili ya wanawake na wanaume, kuimarisha uwezo wao wa kuzalisha mali, na kuongeza kasi ya mageuzi ya muundo wa kiuchumi katika kanda. Ripoti hii inasawiri ni wapi na kwa namna gani maendeleo katika usawa wa jinsia yamefanyika na ni kwa vipi kasi inaweza kuongezwa katika kuendeleza jinsia barani Afrika. Mkazo wake katika usawa wa jinsia unakuja katika kipindi chenye mabadiliko makubwa barani, yakiwemo mageuzi ya hivi karibuni ya mienendo ya kijamii na kiuchumi ambayo imesababisha upigaji hatua mkubwa katika maendeleo ya watu barani Afrika.

Ripoti hii inaonyesha kuungana kwa michakato ya kisiasa na kiuchumi, na inatoa ajenda wazi juu ya kuchukua hatua. Ajenda inatoa njia ya kuzisaidia nchi za Kiafrika kukabili kwa nguvu zaidi changamoto na kuongeza kasi ya maendeleo katika usawa wa jinsia na maendeleo ya wanawake. Ajenda katika usawa wa jinsia inaweza kuunga mkono maendeleo kuelekea Ajenda ya Afrika ya

Licha ya kutambulika vema kwamba wanawake wa Afrika wanaonyesha kupata mafanikio makubwa zaidi kiuchumi na kijamii, manufaa yanayopatikana yanakwenda kwa jamii nzima, lakini kasi ya kuondoa ukosefu wa usawa kwa wanawake bado iko chini.

2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Wakati ambapo Lengo la 5 la SDG linakazia kwa namna ya pekee usawa wa jinsia, kushughulikia masuala ya jinsia kwa nguvu zaidi na kikamilifu kutaharakisha jitihada za serikali na wadau wengine kufikia malengo mengi ya SDG, kama si yote, kwa sababu ya umuhimu na nafasi ambayo wanawake wanashikilia katika jamii na sekta zote.

Licha ya kutambulika vema kwamba wanawake wa Afrika wanaonyesha kupata mafanikio makubwa zaidi kiuchumi na kijamii, manufaa yanayopatikana yanakwenda kwa jamii nzima, lakini kasi ya kuondoa ukosefu wa usawa kwa wanawake bado iko chini.

Njia ya uchambuzi

Kwa mtazamo wa UNDP, usawa wa jinsia kwa jicho la maendeleo ya watu ni jambo linaloshughulikiwa kwa kukuza uwezo wa wanawake na fursa na kuchangia katika kuongeza ubora wa matokeo kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo. Kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo cha 1, kiungo kikuu kati ya usawa wa jinsia na maendeleo ya watu kiko katika masuala matatu yanayoingiliana:

- **Kiuchumi:** kazi inayozalisha zaidi nyumbani na sokoni kama waajiri, waajiriwa na wajasiriamali;
- **Kijamii na kimazingira:** afya bora, elimu, kukomeshwa kwa ukatili wa kimwili na kingono dhidi ya wanawake, na matumizi endelevu kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo; na
- **Kisiasa:** sauti sawa zaidi na uwakilishi katika kutoa uamuzi na upangiliaji rasilimali.

Njia ya kiuchambuzi iliyotumiwa katika ripoti hii ni kuchunguza changamoto ya usawa wa jinsia kwa kuonyesha mwingiliano kati ya michakato ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo ama inakwaza au kuchangia kuendeleza uwezeshaji wanawake. Mtazamo wa ‘uchumi siasa’ unatumika kuelewa namna mawazo, rasilimali na mamlaka yanavyotazamwa, kufanyiwa mapatano na kutekelezwa na makundi tofauti ya kijamii kuhusiana na ukosefu wa usawa wa jinsia—iwe mahali pa kazi, sokoni, au nyumbani.

Ni muhimu kusisitiza kwamba maandalizi ya Ripoti hii ya Maendeleo ya Watu ilihusisha jitihada kubwa za ushirikiano kati ya Ofisi ya Kanda ya UNDP Afrika, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, mashirika ya Umoja wa Mataifa, taasisi za kikanda, watendaji na watafiti. Matokeo yake, siyo tu kwamba inaangazia Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, bali pia nchi za Kiarabu za Afrika ya Kaskazini. Mchakato wa maandalizi ya ripoti hii ulihusisha utafiti wa takwimu na uchambuzi,

taftishi ya nadharia, mashauriano na mashirika mbalimbali kote Afrika, na pia taftishi kupitia mtandao kote barani Afrika.

Sehemu zilizo hapa chini zinaangazia baadhi ya vipengele muhimu vilivyo katika ripoti kamili.

KIELELEZO CHA 1

Usawa wa jinsia na kuimarishwa kwa uwezeshaji wanawake katika kaya, jamii, uchumi na jamii



Chanzo: Imechangiwa na Selim Jahan, Ofisi ya Maendeleo ya Watu (HDRO), 2016.

Ripoti inachunguza changamoto za usawa wa jinsia kwa kuonyesha mwingiliano kati ya michakato ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo au inazuia au kuchangia katika kuendeleza uwezeshaji wanawake.

JEDWALI LA 1

Kulinganisha HDI duniani kwa kutazama kanda

Kada	Wastani wa thamani ya HDI kwa kanda 1990	Wastani wa thamani ya HDI kwa kanda 2000	Wastani wa thamani ya HDI kwa kanda 2014	Mabadiliko katika thamani ya HDI (1990-2014)
Asia Mashariki na Pasifiki	0.516	0.593	0.710	1.34
Ulaya Mashariki na Asia Kati	0.651	0.665	0.748	0.58
Amerika ya Kusini na Karibea	0.625	0.684	0.748	0.75
Asia Kusini	0.437	0.503	0.607	1.38
Afrika	0.426	0.449	0.524	1.09

Chanzo: Imetayarishwa na Timu ya Ripoti ya Maendeleo ya Watu Afrika (AfHDR).

Kwa wastani, wanawake wa Afrika wanafikia tu asilimia 87 ya viwango vya maendeleo vya wanaume.

Upigaji hatua na changamoto katika maendeleo ya watu Afrika

Ripoti inatathmini upigaji hatua katika maendeleo ya watu Afrika kwa kutumia viashiria tofauti ambavyo UNDP imeviandaa ili kupata sura mbalimbali za maendeleo ya watu, ikiwemo kukosekana kwa usawa wa jinsia. Kwa kutumia viashiria hivyo tofauti vya UNDP vya maendeleo ya watu, kuna tofauti kubwa katika thamani na upangaji madaraja kote katika Kanda ya Afrika na kati ya kanda ndogondogo ndani ya Afrika (Jedwali la 1). Kwa ujumla, Afrika ni moja ya viwango vya juu kabisa vya ukuaji katika maendeleo ya watu katika miongo miwili iliyopita, lakini pia ina viwango vya wastani vya chini zaidi vya maendeleo ya watu kulinganisha na kanda nyingine duniani. Wakati huohuo, si nchi zote za Afrika zina maendeleo duni ya watu. Nchi kumi na saba za Kiafrika kote katika kanda ndogo tano zimefikia kiwango cha kati cha maendeleo ya watu – nchi tano Kusini mwa Afrika, tano Afrika ya Kaskazini, nne Afrika ya Kati, mbili Afrika Magharibi, moja Afrika ya Mashariki. Viwango vya juu kabisa vya maendeleo ya watu katika Afrika vinapatikana Aljeria, Libya, Mauritius, Ushelisheli na Tunisia. Nchi thelathini na sita (kati ya 44 kote duniani) zinaingia katika kundi la nchi zenye maendeleo duni ya watu. Nyongeza ya 1 inaonyesha thamani za HDI, nafasi na mienendo katika muda fulani kwa nchi zote za Kiafrika.

Kwa wastani, nchi ambazo mwanzo zilikuwa na viwango vya chini vya maendeleo ya watu zilikua haraka, kwa hiyo kuzifanya zipige hatua kubwa, hadi mwaka 2010 ukuaji huu ulipoanza kupungua. Nchi zifuatazo zilipiga hatua kubwa tangu mwaka 2000:

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Burundi, Mali, Zambia, Niger, Angola, Sierra Leone, Msumbiji, Rwanda na Ethiopia.

Jedwalia 2 ni muhtasari wa wastani wa thamani za kila moja ya kanda ndogo tano za Afrika. Inaangazia tofauti kubwa katika thamani ya HDI miongoni mwa kanda ndogo za Afrika na ndani ya kanda ndogo. Kama ilivyoonyeshwa katika jedwali, Afrika Kaskazini iko juu ya watani wa HDI wa Kanda, na hata pamoja na kujumuishwa kwa Mauritania, iko juu kuliko Asia ya Kusini kwa kulinganisha kote duniani. Kusini mwa Afrika ndiyo kanda ndogo pekee iliyo na thamani ya HDI iliyo juu ya wastani wa kikanda.

Nchi ambazo awali zilikuwa na viwango duni vya maendeleo ya watu zinapiga hatua kubwa. Nchi zifuatazo zimepiga hatua kubwa zaidi tangu mwaka 2000:

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Burundi, Mali, Zambia, Niger, Angola, Sierra Leone, Msumbiji, Rwanda na Ethiopia. Nchi ambazo zilianza na viwango vya chini vya maendeleo ya watu zinakua kwa kasi zaidi, kwa wastani, kuashiria kwamba zinazikaribia zilizotangulia. Hata hivyo, kasi hii imepungua tangu mwaka 2010.

Ukokotoaji kutumia faharisi za jinsia za UNDP zinaonyesha kuna kukosekana kwa usawa wa jinsia kwa kiasi kikubwa karibu katika kila nchi ya Kiafrika. Tofauti ya jinsia katika kipato na vigezo vingine tofauti na kipato husababisha maendeleo ya chini ya watu kwa wanawake kulinganisha na wanaume. Kwa wastani, akina mama wa Kiafrika wanafikia tu asilimia 87 ya maendeleo ya watu wanayopata wanaume.

JEDWALI LA 2

Wastani wa thamani ya HDI kwa kanda ndogo

Kanda ndogo	Thamani ya HDI 1990	Thamani ya HDI 2000	Thamani ya HDI 2014	Mabadiliko katika thamani ya HDI 1990-2014(%)
Afrika Kaskazini	0.533	0.603	0.668	20.209
Afrika Mashariki	0.337	0.403	0.497	32.193
Afrika Magharibi	0.333	0.382	0.461	27.766
Afrika ya Kati	0.453	0.439	0.507	10.651
Kusini mwa Afrika	0.481	0.478	0.570	15.614
Wastani wa thamani ya HDI kwa Kanda ya Afrika	0.426	0.449	0.524	18.702

Chanzo: Imeandaliwa na Timu ya AfHDR

Serikali za Kiafrika zinatambua wazi juu ya masuala yanayoathiri hadhi ya wanawake na vilevile aina ya sera na programu ambazo zingeweza kuleta tofauti, lakini uelekezaji wa bajeti ili kusaidia sera na programu muhimu umepungua hadi chini ya viwango vilivyowekwa na Umoja wa Afrika kwa matumizi ya sekta za jamii.

Masuala ya kijamii kuhusu usawa wa jinsia

Masuala ya kijamii kuhusu usawa wa jinsia, ambayo yanahusu mienendo katika afya na elimu, ni vigezo muhimu vya kupima usawa na uwezeshaji wanawake. Kwa ujumla, ukosefu wa usawa wa jinsia unamaanisha upungufu wa fursa kwa ustawi wa wanawake katika jamii fulani kwa ujumla wake. Katika miongo iliyopita, uwezo wa raia umepanuka katika nchi nyingi za Afrika katika maeneo ya msingi kama vile afya, elimu na huduma nyingine za jamii. Maendeleo haya yamejumuisha wanawake na wasichana, ambao leo, wana nafasi kubwa zaidi ya kupata elimu katika ngazi zote, huduma bora za afya, kuzaa watoto kwa usalama, na kuwa na maisha marefu zaidi.

Wanawake wanakabiliana na vikwazo vikali katika afya zao hasa kwa sababu ya masuala kama ndoa za mapema (Kielelezo cha 2), ukatili wa kingono na kimwili, na kuendelea kutokea kwa vifo vya akina mama wajawazito. Wanawake walio hatarini zaidi ni wale walio katika umri wa kuzaa. Kutokea kwa uzazi miongoni mwa vijana wa umri wa balehe katika nchi nyingi ni jambo linalopunguza kasi ya upigaji hatua katika maendeleo ya watu. Kwa mfano, ongezeko la asilimia moja katika viwango vya uzazi miongoni mwa vijana wa umri wa balehe hupunguza HDI kwa takribani asilimia 1.1.

Suala la ukatili linalowaathiri wanawake linajumuisha ukatili wa majumbani, ukatili kati ya wapenzi, ubakaji, ukeketaji, vitisho, na ongezeko la vitisho dhidi ya usalama binafsi wa wanawake nyakati za vita na machafuko.

Kuhusiana na elimu, inatia moyo kwamba karibu usawa wa jinsia umefikiwa katika uandikishaji watoto katika shule za msingi. Hata hivyo, ubaguzi

Matokeo yasiyo linganifu katika afya na elimu bado yanaonekana katika kanda mbalimbali na kati ya nchi na nchi. Ukosefu wa usawa wa jinsia katika huduma za jamii unamaanisha fursa za chini kwa ustawi wa wanawake kwa namna ya pekee na kwa jamii nzima kwa ujumla.

KIELELEZO CHA 2

Viwango vya ndoa za utotoni katika kanda ndogo (%), 2005-2013



Chanzo: Imeandwaliwa na Timu ya AfHDR kwa kutumia taarifa za ulimwengu katika hazina ya data ya UNICEF 2015.

JEDWALI LA 3

Ushiriki wa wanawake katika ajira zisizohusisha kilimo, sekta isiyo rasmi

Nchi	Mwaka wa utafiti	% ya Ajira ya wanawake katika shughuli zisizo za kilimo na sekta isiyo rasmi
Mauritius	2009	6.7
Afrika ya Kusini	2010	16.8
Lesotho	2008	48.1
Ethiopia (mijini)	2004	47.9
Zimbabwe	2004	53.1
Liberia	2010	65.4
Ivory Coast	2008	82.8
Zambia	2008	70.3
Madagascar	2009	63.8
Uganda	2010	62.2
Tanzania (Jamhuri ya Muungano)	2005/06	49.8
Mali	2004	79.6
Mali	2004	74

Imeandaliwa na Timu ya AfHDR kutoka ILO, 2014. Wakina Mama na Wakina Baba Kazini: Sheria na Taratibu kote Duniani. Geneva.

wa jinsia bado ni mkubwa katika elimu ya sekondari na elimu ya juu. Sababu zinazofanya watoto wasihudhurie shule zinatofautiana, lakini mara nyingi zinahusishwa na umaskini, asili ya kinasaba, kutengwa kijamii, kuishi katika maeneo ya vijijini au makazi duni, umbali wa kijiografia, majanga, mapigano, kukosekana kwa huduma za msingi na viwango duni vya elimu.

Vikwazo hivi mara nyingi huingiliana na jinsia katika kutengeneza vikwazo zaidi katika fursa ya kujifunza. Yote haya yanasababisha wastani wa chini wa miaka ya kuwa shuleni katika kanda ndogo mbalimbali

Habari njema ni kwamba nchi ambamo idadi kubwa ya wanawake wamepata walau elimu ya sekondari kwa kawaida huwa na matokeo bora katika HDI.

KIELELEZO CHA 3

Wastani wa miaka ya kuwa shuleni, watu wa umri wa miaka 25 na zaidi, kwa jinsi na kanda ndogo, 2014



Chanzo: Imekokotolewa na Timu ya AfHDR kwa kutumia data za Ripoti ya Maendeleo ya Watu 2015 ya UNDP, New York, Marekani

Wanawake katika uchumi wa Kiafrika

Kigezo kingine muhimu cha usawa wa jinsia kinaonyeshwa na wanawake walio makazini na utoaji uamuzi katika masuala ya kiuchumi. Tofauti kubwa za kiuchumi na mahali pa kazi kati ya wanaume na wanawake bado zinaendelea kuwa ndio kawaida badala ya jambo la pekee katika nchi nyingi za Kiafrika. Ukosefu huu wa usawa unaonekana kote Afrika katika kupata mali za kiuchumi, ushiriki katika mahali pa kazi, fursa za ujasiriamali, na matumizi na manufaa ya rasilimali na mazingira.

Kwa kuongezea, kuna uwezekano mkubwa zaidi wa kuwakuta wanawake katika ajira zenye hatari na zenye kanuni mbovu na pasipo na kinga ya kijamii ya uhakika kwa sababu ya tofauti katika elimu na kukosekana ulinganifu kati ya stadi za wanawake na zile zinazotakiwa katika soko la ajira.

Matokeo yake ni kuwa wanawake husukumwa kubaki katika ajira isiyo rasmi. Inakadiriwa, kwa kutumia data za utafiti za 2004 hadi 2010, kwamba ushiriki wa ajira zisizotokana na kilimo zisizo rasmi katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ni karibu asilimia 66 ya ajira zote za wanawake. Hii hutofautiana kutoka nchi hadi nchi (Jedwali la 3).

Kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika soko la ajira hakujamaanisha kuongezeka kwa fursa katika kazi au biashara zinazolipa vizuri. Tofauti ya mshahara nje ya sekta ya kilimo ni kubwa katika masoko yote ya ajira Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambako, kwa wastani, tofauti ya malipo kwa jinsia inakadiriwa kuwa asilimia 30.

Kwa hiyo, kwa kila dola 1 ya Marekani anayopata mwanaume katika sekta za viwanda, huduma na biashara, wanawake wanalipwa senti 70 za dola. Tofauti katika mapato kati ya wanawake na wanaume inaathiriwa na vigezo kama vile umri, aina ya kazi, elimu, wazazi na ndoa.

Kwa sababu mapokeo ya kijamii na imani huwapangia wanawake na wasichana wa Kiafrika wajibu wa msingi wa kushughulika na kazi za nyumbani, wanawake, kwa wastani, wanatumia muda mara mbili zaidi ya wanaume katika kazi za nyumbani – kulea watoto na wazee, kupika, kufua, na kuchoa maji na kusenya kuni.

Tofauti kubwa za kiuchumi na mahali pa kazi kati ya wanaume na wanawake wa Kiafrika bado inaendelea kuwa kawaida badala ya jambo la pekee. Tofauti hizi ziko katika Kanda nzima ya Afrika kwa maana ya kupata mali za kiuchumi, ushiriki katika mahali pa kazi, fursa za ujasiriamali, na matumizi na manufaa kutoka katika rasilimali za asili na mazingira.

Katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, asilimia 71 ya mzigo wa kuteka maji kwa ajili ya kaya unawaangukia wanawake na wasichana.

Kadiri hadhi ya kiuchumi ya wanawake inavyoimarika ndivyo familia nzima pia inavyokuwa na hali bora – kigezo kikuu kupunguza makali ya umaskini wa kurithiwa kutoka kizazi hadi kizazi na maendeleo duni ya watu. Kwa mfano, umiliki wa hati za ardhi unawasilisha chanzo muhimu cha usawa sawia na amana kwa wanawake kuweza kupata mikopo na kupata aina nyingine za mali zenye kuingiza kipato. Kukosa nafasi ya kumiliki ardhi huwakosesha wanawake wa Kiafrika zana muhimu ya kiuchumi ya kupanua njia zao za kujipatia riziki.

Kuna gharama kubwa kiuchumi pale wanawake wanaponyimwa fursa ya kushiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa mataifa yao. Kwa mujibu wa ripoti hii, hasara ya kiuchumi kwa sababu ya tofauti za jinsia kati ya 2010 na 2014 inakadiriwa kupita dola za Marekani bilioni 90 katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, na kufikia kilele cha takribani dola za Marekani bilioni 105 katika mwaka 2014. Matokeo haya yanathibitisha kwamba Afrika inapoteza uwezo wake wa kukua kikamilifu kwa sababu sehemu kubwa ya akiba ya ukuaji wake – wanawake – haitumiki ipasavyo.

Wanawake wa Kiafrika katika siasa na uongozi

Msukumo mwingine muhimu katika kuleta usawa wa jinsia ni nafasi ya sauti ya kisiasa na uongozi ya mwanamke. Kwa muda mrefu ushiriki wa wanawake katika siasa na uwakilishi kwenye utawala vimechukuliwa kama viashiria muhimu vya ngazi ya jumla vya ufanisi na uwajibikaji katika nchi.

Kwa kiwango kile ambapo wanawake zaidi wanahusishwa katika nafasi za siasa na uongozi, kuna maana kwamba haki za wanawake, vipaumbele, mahitaji na maslahi yao hayawezi kupuuzwa au kunyamaziwa kabisa (Kielelezo cha 4).

Hatua muhimu imepigwa katika kuendeleza ushiriki wa wanawake katika kushika nafasi za kuchaguliwa na katika nafasi za uongozi kwenye sekta za umma na binafsi.

Upigaji hatua wa jumla katika ngazi ya siasa na uongozi iko chini sana kulinganisha na kinachotakiwa ili kuonyesha athari katika kufikia usawa kamili wa jinsia katika nchi za Kiafrika. Miundo iliyopo ya kijamii na kisiasa bado inazuia utumiaji wa uwezo kamili wa wanawake katika kusaidia kwa usawa kuongoza siasa za kitaifa na mahalia na ajenda ya sera.

Kwa wastani, hasara kwa mwaka katika Pato Ghafi kati ya mwaka 2010 na 2014, kwa sababu ya tofauti ya jinsia katika soko la ajira, ilipita dola za Marekani bilioni 90, na kufikia kilele cha karibu dola za Marekani bilioni 105 mwaka 2014 katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kupunguza tofauti ya jinsia katika uendeshaji masuala ya umma kunasaidia kuhakikisha utawala wa kidemokrasi, kurejesha imani katika taasisi za umma, na kuharakisha uwajibikaji katika sera na programu za serikali.

KIELELEZO CHA 4

Vichocheo vya kuongeza ushiriki wa wanawake katika siasa barani Afrika



Baadhi ya nchi zimefanikiwa sana katika kuchagua wanawake kuingia kwenye mabunge yao na nafasi nyingine za kuchaguliwa, lakini miundo iliyopo ya kijamii na kisiasa bado inazuia uwezo kamili wa wanawake katika kusaidia kujenga kwa usawa ajenda ya kitaifa na mahalia ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Zaidi ya siasa, wanawake pia wamepiga hatua katika nafasi za uongozi katika maeneo kama vile utumishi wa umma, vyama vya wafanyakazi na sekta binafsi, lakini hata huku upigaji hatua katika kufikia usawa wa jinsia bado uko nyuma kwa sababu ya vikwazo katika kuleta mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Katika sekta binafsi, mtazamo wa jumla kwamba shughuli za wanaume zinazidi zile za wanawake hauonyeshwi kwa kutumia data wala hautoi sababu ya kuwepo tofauti katika uongozi. Ingawa hali inaimarika, asilimia ya makampuni ambayo mameneja wake ni wanawake bado iko kati ya 7 na 30. Kupunguza tofauti ya uongozi katika sekta binafsi kunategemea ongezeko katika wingi wa wanawake wenye elimu ya ngazi ya chuo katika maeneo yanayohusiana na sayansi na teknolojia.

Michakato ya kisiasa ni eneo lingine kuu katika kutoa uamuzi na katika kutekeleza mamlaka na ushawishi. Kihistoria, ushiriki wa wanawake umekuwa mdogo licha ya wingi wa mikataba ya makubaliano ya amani katika bara zima.

Katika muongo mmoja uliopita, kumekuwa na mabadiliko makubwa katika nafasi ya wanawake kwenye kutatua migogoro na kujenga amani kutoka katika kushawishi kwa njia zisizo rasmi mapatano ya kukomesha uadui au makubaliano ya amani.

Kuna ongezeko la kukubalika zaidi kwamba wanawake wanapaswa kuwa sehemu muhimu na rasmi ya mchakato wowote wa mapatano ya amani, hasa kwa kuzingatia nafasi yao katika kupata na kulinda amani.

Nafasi ya sheria na mapokeo ya kijamii katika usawa wa jinsia

Sheria na mapokeo ya kijamii iliyopo, na namna haya yanavyoingiliana yana athari kubwa katika usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake. Msingi wa umuhimu wa kisheria na mapokeo ya kijamii hauwezi kusisitizwa zaidi katika maeneo kama vile upatikanaji wa huduma za kijamii, afya na elimu, na vilevile nafasi yao katika kuleta ushawishi kwenye ukatili kwa misingi ya jinsia, ndoa za utotoni na vikwazo vingine vya kijamii na kitamaduni katika kuleta usawa wa jinsia (tazama Kielelezo cha 5).

Nchi za Afrika na maeneo ya kikanda yameanzisha mifumo mbalimbali ya kisheria, maeneo ya kupigiwa mfano na utungwaji seria ili kuhimiza usawa wa jinsia. Changamoto haiko katika kurekebisha viwango vya kisheria vya sasa, bali katika kuhakikisha kwamba viwango vinatangazwa, kukubaliwa na kuingizwa sheria na kanuni za kitaifa na kisha kutekelezwa na kusimamiwa kikamilifu.

Changamoto haiko katika kurekebisha viwango vya kisheria vya sasa, bali katika kuhakikisha kwamba viwango vinatangazwa, kukubaliwa na kuingizwa sheria na kanuni za kitaifa na kisha kutekelezwa na kusimamiwa kikamilifu

KIELELEZO CHA 5

Idadi ya nchi za Kiafrika zenye sheria zisizo za ubaguzi wa jinsia, 2014



Chanzo: Imeandaliwa na Timu ya AfHDR kwa kutumia World Bank, 2015a

Ukimya wa kijamii na kitaasisi kwenye ukatili dhidi ya wanawake unaungana na kuendeleza ukatili wa kimfumo na uliochukuliwa kuwa kawaida katika Afrika.

Tathmini za sheria za sasa zinazozingatia jinsia katika maeneo ya sheria za familia, sheria za ardhi, sheria za kazi na ajira na sheria za kimila ni muhimu katika kubaini na kuondoa ubaguzi unaoendelea kwa msingi wa jinsia.

Mapokeo mengi ya kijamii yameendelea kuwa na taathira hasi katika kufikiwa kwa usawa wa jinsia katika Afrika. Licha ya kuwepo kwa sheria za kimataifa na kikanda na matamko kuhusiana na haki za binadamu na usawa wa jinsia, viwango hivi mara nyingi vinapingwa au kukomeshwa katika ngazi za kitaifa na kijamii kwa sababu ya mapokeo ya kijamii ambayo ni vigumu kuyaepa.

Ni tofauti kati ya haki za kisheria na matarajio, kwa upande mmoja, na taratibu zilizozoeleka na tabia zilizojikita katika mapokeo ya kijamii na kijadi, kwa upande mwingine, ambayo yanaleta changamoto ya hatari katika kuongeza kasi ya usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake.

Mapokeo mengi ya kijamii yana nafasi muhimu sana na chanya katika kuunda familia madhubuti na kuleta mshikamano wa kijamii, na pia kuanzisha mazingira ya kuaminiana na kusaidiana katika nyakati za migogoro na ngumu. Hata hivyo, mapokeo mengine ya kijamii, yanaendelea kuwa na athari mbaya katika kufikiwa kwa usawa wa jinsia, licha ya kuwepo kwa sheria na viwango vilivyokubalika.

Mapokeo ya kijamii kama hayo na dhana potofu za jinsia ambazo zinasababisha misimamo, wajibu na upendeleo tofauti kwa wanawake na wanaume yanazuia upigaji hatua kuelekea kwenye usawa wa jinsia. Kwa mujibu wa utafiti wa Afrobarometer wa 2015, takribani robo moja ya Waafrika hawakubaliani na dhana ya usawa wa jinsia, ndiyo kusema, wanapingana au wanapinga kabisa dhana ya msingi wa haki sawa kati ya wanaume na wanawake. Hali hii inataka utayari wa kueneza uelewa na utetezi kuhusu misukumo ya usawa wa jinsia katika Afrika.

Taathari ya mapokeo ya kijamii yanayowabana wanawake pia imeonekana kuwa na athari mbaya kwa wanaume na wavulana, na jamii kwa ujumla, ambapo kimsingi humzuia kila mmoja na kumfanya asifikie maendeleo ya watu ya kiwango cha juu na kuzuia jamii kutofikia uwezo wao kamili wa maendeleo.

Njia za sera na programu za kushughulikia kutokuwepo kwa usawa wa jinsia

Serikali za Afrika zimetumia njia mbalimbali za sera na programu ili kushughulikia kukosekana kwa usawa wa jinsia. Hizi ni pamoja na jitihada katika ngazi pana na kisekta ambazo zimelenga kushughulikia ukosefu wa usawa wa jinsia kupitia muunganiko wa sera na taasisi mbalimbali. Mifano ni pamoja na sera za fedha (ikiwemo ya matumizi ya umma na ruzuku), hatua za kisheria na kikanuni na kuweka kando programu, na pia hatua nyingine zilizolengwa. Hata hivyo, rekodi za mafanikio ni mchanganyiko, na kuna nafasi ya kutosha kuongeza jitihada hizo, kwa upana na kina cha jitihada. Kwa sababu hii, kuna mengi sana ya kujifunza kutoka katika uzoefu wa Amerika ya Kusini na bara Asia.

Nchi nyingi za Kiafrika zimefuata utaratibu wa kimataifa kwa kuanzisha taasisi kwa ajili ya ustawi wa wanawake. Njia hizi mpya za kitaasisi katika masuala ya jinsia zimechukua sura nyingi, ikiwemo wizara zinazohusika au idara za wizara za wanawake,

KIELELEZO CHA 6

Njia za sera na kitaasisi za kuleta usawa wa jinsia



Chanzo: Imechukuliwa kutoka katika WHO Trends in Maternity Mortality: 1990 hadi 2015, Geneva.

Nchi za Kiafrika zimetumia sera na njia za kitaasisi ili kuhamasisha usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake. Lakini rekodi za mafanikio zinatofautiana, na kuna nafasi kubwa ya kuongeza bidii ya jitihada kwa mapana na marefu. Kwa sababu hii, kuna mengi ya kujifunza kutoka katika uzoefu wa kanda nyingine, kama vile Amerika ya Kusini na Karibea.

ambazo katika baadhi ya nchi zimefanywa kuwa njia za taasisi zinazoongoza.

Suala la kuanzisha modeli za kitaasisi zenye ufanisi katika kuwa na jamii iliyo sawa zaidi ni muhimu lieleweke kama wajibu wa wote katika wizara mbalimbali na kuhusisha sekta binafsi na vyama vya kiraia (Kielelezo cha 6).

Serikali za Kiafrika zimeanza kutumia programu mbalimbali za hifadhi ya jamii (zikiwemo utoaji fedha taslimu na ruzuku) ili kuhamasisha usawa wa jinsia na kupunguza umaskini. Hata hivyo, bado kuna nafasi ya kupanua zaidi programu za utoaji fedha taslimu na huduma za jamii ambazo zitaleta mabadiliko ya moja kwa moja katika kuboresha ustawi wa kiuchumi na kijamii wa wanawake. Hizi ni pamoja na likizo za uzazi, utoaji wa matunzo kwa watoto, na aina fulani ya msaada wa kipato au fedha taslimu kwa kazi zisizolipwa wanazofanya wanawake, ambazo kwa kawaida hufanywa nyumbani au mashambani.

Vilevile, mazingira ya kisheria ambamo kwamo wanawake na wanaume wanashughulika katika jamii inaonyesha ukweli kwamba taasisi zenye ufanisi zaidi zisizo za ubaguzi, sera zilizo rafiki kwa familia na viwango vya mazingira ya kazi vingeweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza madhira ya wanawake kiuchumi na kijamii (Kielelezo cha 7). Katika makadirio ya asilimia 28 ya nchi za Kiafrika, sheria za kimila zinachukuliwa kuwa ni chanzo sahihi cha sheria—hata kama inakiuka vipengele vya kikatiba kuhusu masuala ya kutobaguana na usawa.

Ili kutumia vizuri mapokeo ya kisheria ya kimataifa na kikanda kwa ajili ya usawa wa jinsia, nchi nyingi za Kiafrika, kwa hiyo, zinaweza kufafanua kwa ubayana zaidi, kutekeleza na kusimamia sheria zilizopo, taratibu na kanuni ambazo zote zinaweza kuwa na athari kuba katika kuimarisha upatikanaji wa haki na mastahili kwa wanawake. Kuoanisha

KIELELEZO CHA 7

Ushirikiano wa kitaasisi ili kuleta usawa wa jinsia



Chanzo: Imesanifiwa na Timu ya AfHDR

sheria na kanuni za nchi na sheria zile za kimila na kijadi bado ni changamoto kubwa.

Ajenda ya kuchukua hatua kuharakisha usawa wa jinsia

Taasisi za umma na binafsi na vilevile vyama vya kiraia vinapaswa kujidhatiti kutekeleza viwango vya ithibati vya Makubaliano ya Usawa wa Jinsia.

Ripoti ya Maendeleo ya Watu Afrika ya 2016 inatoa mahitimisho muhimu na ujumbe mkuu ambao unaweka muundo kazi wa kimkakati na ajenda ya uchukuaji hatua inayolenga njia yenye mwelekeo zaidi wa matokeo na iliyo kamili katika kushughulikia ukosefu wa usawa wa jinsia. 'Njia' nne pana zimependekezwa ambazo zinatoa miongozo ya sera na programu ili kuharakisha usawa wa jinsia na kuunganisha vema jinsia katika ajenda pana zaidi ya maendeleo ya watu na kusaidia kufikiwa kwa SDGs na Ajenda ya Afrika ya 2063. Njia hizo nne zimeonyeshwa katika Kielelezo cha 8 na kuangaziwa zaidi hapa chini.

Hizi njia nne zinamaanisha:

Njia ya 1: ***Kusaidia upitishaji wa mabadiliko ya kisheria,*** sera na kanuni ili kuendeleza uwezeshaji wanawake kupitia utengenezaji na utekelezaji kamili wa muunganiko wa sheria na kanuni, sera na

programu ambazo zinatoa fursa sawa kwa wote, bila kujali jinsi yao.

Njia ya 2: Kusaidia uwezo wa taifa kuhamasisha na kuongeza ushiriki na uongozi wa wanawake katika kutoa uamuzi nyumbani, katika uchumi na jamii, kitu kinachoweza kusaidia kukabili masuala yanayoendeleza ubaguzi wa kijamii na kiuchumi, umaskini na kukosekana kwa usawa nyumbani, katika uchumi na masoko, na katika jamii. Kwa sababu hii, taasisi za umma na binafsi na pia vyama vya kiraia (CSOs) havina budi kuweka nia thabiti kutekeleza viwango vya ithibati vya UNDP yaani Ithibati ya Usawa wa Jinsia ili kuleta matokeo ya usawa wa jinsia yanayoleta mageuzi barani Afrika.

Njia ya 3: Kusaidia uwezo wa kutekeleza mikabala kutoka katika sekta mtambuka ili kupunguza makali ya athari za vitendo vya kibaguzi katika afya na elimu, jambo linaloweza kuzaa ushirikiano kati ya wizara na wizara na sekta binafsi na vyama vya kiraia.

Njia ya 4: *Kuwasaidia wanawake* ***kupata umiliki na usimamizi wa mali za kiuchumi na kimazingira,*** jambo linaloweza kukabili masuala yanayoendeleza ubaguzi wa kijamii-kiuchumi, umaskini na kukosekana kwa usawa. Hii inajumuisha kuanzishwa kwa Benki ya Uwekezaji ya Wanawake Afrika na kufungua fursa za uwekezaji katika benki za maendeleo.

Kwa kuzingatia njia hizi nne, kuna swali kubwa la kimkakati linalozikabili serikali za Kiafrika zinazotaka kuongeza kasi ya haki na mastahili ya wanawake:

Wakipata ahadi thabiti ya kisiasa ya kufanya hivyo, je, viongozi wa Kiafrika na watunga sera wanaweza vipi kwa kukabili kwa nguvu zaidi ukosefu wa usawa wa kijinsia katikati ya vipaumbele vingine vya kitaifa vinavyoshindana?

Kwa sababu ya mambo mengi yanayowakabili viongozi na watunga sera kuendeleza kasi ya ukuaji kiuchumi, kutawanya uchumi kwa ajili ya kuunganishwa na masoko ya ulimwengu, kutafuta mahitaji yanayokua kwa kasi ya watu wa daraja la kati linalopanuka haraka, kushughulikia mitikisiko na hatari zinazojitokeza, kushughulikia masuala ya kiusalama, maamuzi magumu lazima daima yafanywe katika kugombania matumizi ya rasilimali chache zilizopo.

Ili kutoa mwongozo wa sera kwa viongozi wa Afrika wanaohusika na njiapanda zilizopo, maeneo sita ya kimkakati yanapendekezwa kama miundodhana ya kitaasisi kwa ajili ya uchukuaji hatua katika kushughulikia ukosefu wa usawa katika jinsia. Muundodhana huu unaendana na hoja ya kuweka mbele ule uongezaji kasi wa usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake

KIELELEZO CHA 8

Njia za kimkakati za kushughulikia kukosekana kwa usawa wa jinsia



Source: Adapted from Changing with the World: UNDP Strategic Plan 2014-2017. New York.

sambamba unawakilisha njia ya vitendo ya uendeshaji mambo kwa ajili ya Serikali za Afrika kukabili changamoto za kufikia SDGs na kuendelea na Ajenda ya Umoja wa Afrika ya 2063.

Kushughulikia usawa wa jinsia si tofauti na kushughulikia malengo ya SDGs. Kwa hiyo, kadiri masuala ya ukosefu wa jinsia yanavyoshughulikiwa, basi maendeleo yanafanyika katika eneo zima la malengo ya maendeleo kama yanayoainishwa katika SDGs.

Kwa mtazamo huu, maeneo sita ya kimkakati ya kuzingatia yanafafanuliwa hapa chini.

Kutumia usawa wa jinsia kama lensi ya kuongozea sera kwa ajili ya utungwaji, upangaji na utekelezaji wa ajenda ya maendeleo. Ni fikra potofu kudhani kwamba kwa kutoa kipaumbele cha juu kwa usawa wa jinsia kuna maana ya kutotoa nafasi kwa vipaumbele vingine vya maendeleo. Kukazia masuala ya jinsia hakuna ya uchaguzi wa kupoteza kwingine, ambapo kuchagua kipaumbele kimoja kinaondoa vingine. Bila kujali lengo la sera—ukuaji jumuishi na mtawanyiko wa uchumi, kuhuisha sekta ya kilimo, kuongeza ubora wa huduma za kitaifa za afya na elimu, kuondoa umaskini mkali, kukabili mabadiliko ya tabia ya nchi—endapo asilimia 50 ya watu, yaani, wanawake na wasichana, hawanufaiki kwa usawa kutokana na sera na programu, basi hiyo ya mwanzo haiwezi kuchukuliwa kuwa mafanikio. Ili kuondoa dhana hii potofu na kushughulikia usawa wa jinsia siyo tena kuhusu 'kuongeza' katika sera na programu maalumu kwa ajili ya wanawake au kuwa na wizara na wakala tofauti za wanawake, bali, badala yake ni kuhakikisha kwamba sera na programu zote zinakusudiwa kufikia matokeo sawa kwa wanaume na wanawake.

Kukabili mapokeo potofu ya kijamii moja kwa moja. Si kuchukulia mambo kiurahisi kwamba kubadili mapokeo ya kijamii yanayozuia fursa sawa za wanawake na wasichana utakuwa mchakato wa muda mrefu na mgumu. Kufanya bidii katika kubomoa mapokeo hasi ya kijamii na vikwazo vya kijadi kwa hakika ni jambo zito kimaadili, gumu

Kuanzishwa kwa Benki ya Uwekezaji ya Wanawake Afrika ni jambo muhimu.

kijamii na hatari kisiasa katika utekelezaji wake, au kwa usahihi, uchukuaji hatua mtambuka. Viongozi wa Kiafrika na watunga sera kwa hiyo wanahitaji kuelewa asili ya kubomoa mapokeo ya kijamii yaliyo hasi na kuyabadili kwa mapokeo chanya ya kijamii. Mara nyingi, njia itakuwa na maana ya kutafuta upatanisho kati ya sheria na mapokeo ya kijamii.

Kutumia mipango na bajeti ili kuweka kipaumbele kwa usawa wa jinsia. Serikali za Kiafrika bila shaka zitakuwa hazina budi kubaini na kutekeleza uchaguzi wa seti za sera na programu mkakati ambao unaonekana kuwa kipaumbele katika muktadha wa kitaifa, ambao una uwezekano wa juu wa kufanya mabadiliko muhimu, ambayo inaweza kufanya kazi pamoja, na ambayo yana nafasi kubwa ya kutekelezwa kwa mafanikio. Lengo ni kupendekeza kwamba serikali za Kiafrika ni lazima ziwe na mchakato wa uwekaji vipaumbele vya kuleta usawa wa jinsia, hasa kwa sababu ya mahitaji makubwa na upungufu wa rasilimali zinazokabili kila nchi. Jukumu hili halina maana ya kuchagua na kutekeleza wigo mpana wa uchaguzi wa sera, bali badala yake, kuweka kipaumbele, kwa utaratibu mzuri na mchakato wa wazi, miongoni mwa (na mara nyingi zinazoshindana) uchaguzi wa sera—ambazo kwazo zote zinashindania rasilimali chache za umma zilizopo.

Maswali matatu ya mwongozo yanapendekezwa kwa ajili ya kuunganisha vipaumbele vya muda mfupi na mrefu:

Je, ni sera na programu zipi zina uwezekano wa kuongeza ubora wa maisha ya wanawake na kuwaingiza katika mkondo mkuu wa uchumi kupitia fursa za ajira zenye tija na kuboreshwa kwa ustawi wa jamii?

- Ni kwa njia zipi maoni na masuala ya wanawake, wadau na wanufaika wengine yanaingizwa katika mchakato wa kutoa uamuzi?
- Katika hali ambapo rasilimali zinahamishwa kutoka programu au jitihada moja hadi nyingine, je, uhamishaji huu unaweza kukubaliwa kwa maana ya kuleta matokeo bora zaidi ya kiuchumi na kijamii kwa wanawake na wasichana kuliko ambavyo pengine mambo yangekuwa?

Kuimarisha sera wezeshi na uwezo wa kitaasisi. Kuleta usawa wa jinsia na kuongeza kasi ya maendeleo ya watu kutahitaji serikali za Kiafrika kuweka nia thabiti katika muundodhana imara, unaolenga mabadiliko na wenye uwajibikaji, unaoendeleza sera kwa ajili ya sekta za umma na binafsi kwa kuzingatia dira na uongozi wa muda mrefu, mapokeo na tunu za pamoja, na sheria na taasisi ambazo zinajenga kuaminiana na mshikamano.

Ukusanyaji na uchambuzi wa data haupaswi kuchukuliwa kama jambo lililokuja baadae, bali kama kazi muhimu ya huduma za serikali, ambayo inahitaji fedha nyingi na uungwaji mkono kisiasa.

Kama maendeleo yasipounganishwa na jinsia basi yanakuwa hatarini. Sera na programu zote hazina budi kukusudiwa kufikia matokeo sawa kwa wanaume na wanawake.

Wakati huohuo, serikali zitahitaji uwezo wa kuwa tayari kupokea mabadiliko na kuendana nayo. Katika jamii zenye mambo mengi kama za Afrika, matokeo ya sera fulani huwa mara nyingi hayatabiriki. Serikali za Afrika zitahitaji kufuata muundodhana wa utawala ambao unalenga kutoa matokeo na kutatua matatizo na kuendana kwa pamoja na kwa haraka—kinyume na kuacha njia ya uchukuaji hatua kwa madhara ambayo hayakukusudiwa.

Kuongeza thamani katika data ili kuimarisha utoaji uamuzi. Ili serikali za Kiafrika zishughulikie kikamilifu utoati wa jinsia na kuelewa matokeo ya sera na programu zilizochaguliwa, ukusanyaji data wa nguvu zaidi na mifumo ya usimamizi itahitajika. Uwezo wenye tija katika takwimu na usimamizi na tathamini ndiyo 'vilainishi' ambavyo kwavyo serikali zinaweza kutenda kama dola linaloweza kupokea mabadiliko na kufanya mabadiliko ya lazima na masahihisho wakati wa utekelezaji. Ukusanyaji na uchambuzi data haupaswi kutazamwa kama jambo la baadaye, bali kama kazi muhimu ya huduma za serikali, ambayo inahitaji msaada wa kifedha na kisiasa. Kutathmini uwezo wa kusimamia mipango na bajeti za kitaifa za maendeleo na SDGs, pamoja na takwimu za kawaida za kiuchumi na kijamii, ni jambo la lazima. Hii inawasilisha fursa ya pekee kwa serikali za Kiafrika kutathmini jinsi wakala za takwimu na wizara zinazohusika zinavyoweza kuimarisha ukusanyaji wa wa data, kuzisimamia na kuzichambua ili kupata athari kamili katika jinsia kwa sera na jitihada za sasa, na jinsi, kadiri muda unavyopita, zinazoweza kuongezewa ubora.

Kuweka kipaumbele kwa ushirikiano wa kikanda na wa Nchi za Kusini. Ni muhimu kuweka uzito katika umuhimu wa Ushirikiano wa Kikanda na Nchi za Kusini katika kusanifu na kutekeleza sera na jitihada zinazokazia jinsia. Nchi za Kiafrika zina mambo mengi ya kujifuza miongoni mwao—kupitia yale ambayo yameleta matunda na ambayo hayakufanikiwa. Pia kuna mafunzo mengi yanayoweza kupatikana kutoka katika uzoefu wa nchi za Amerika ya Kusini na Karibea. Mkazo wa ushirikiano huo hauna budi kuwa zana ya kushirikishana, mikakati na uzoefu katika sekta zote, kutoka miradi mikubwa ya miundombinu hadi hatua katika ngazi ya jamii za kutatua matatizo – yote yakihitaji kusukuma ubunifu, kujifunza na kufanya upanuzi. Kuna uwezekano mkubwa wa kupanua mafunzo katika ngazi ya nchi nzima na ziara za mafunzo, kupeleka wafanyakazi kwenda kujifunza na fursa nyingine za kujifunza kwa kuona ambazo zinawaweka mameneja na watunga sera moja kwa moja katika kiini cha mabadiliko ya mahali.

Hitimisho

Kwa muhtasari, ripoti inakazia kuendelea kuwepo kwa tatizo la usawa wa jinsia ambalo linawakabili wanawake na wasichana wa Afrika. Hitimisho muhimu ni kwamba usawa wa jinsia hauwezi kupatikana kwa kuwa na wizara maalumu kwa ajili ya masuala ya jinsia au miradi na programu za wanawake pekee (ingawa zinaweza kuwa muhimu), bali hasa, kwa kushughulikia usawa wa jinsia kama jitihada pana katika sekta mtambuka ambazo zinahusisha makundi yote katika jamii. Ripoti inazidi kusisitiza mwingiliano kati ya ustawi wa wanawake na fursa zao za kiuchumi kwa ajili ya maisha yenye tija zaidi. Kusisitiza jitihada zote hizi itakuwa jukumu la lazima lakini ambalo linaeleweka kwamba litakuwa gumu la kuvunjilia mbali mapokeo ya kijamii na vikwazo vya kijadi vyenye madhara ambavyo vina athari mbaya kwa wanawake masikini na familia zao.

Hitimisho lingine ni kwamba, kuongeza kasi ya usawa wa jinsia kutakuwa na maana ya jitihada kubwa za ushirikiano unaohusisha sit u serikali za kitaifa na za mitaa, bali pia asasi zisizo za serikali, sekta binafsi, makundi ya utetezi na asasi za kuleta tija katika jamii.

Hatimaye, serikali za Kiafrika hazina budi kueleza bayana vigezo vikuu vya kupima maendeleo, kufanya marekebisho kama inavyotakiwa na kuendeleza dira ya taifa ya matokeo muhimu ambayo kuleta usawa wa jinsia kunaweza kuipatia jamii nzima. Watu wa Afrika hawana budi wao na serikali zao kuwajibika kwa kupiga hatua katika maendeleo ndani ya muda uliopangwa ambao haupunguzi uharaka unaotakiwa katika kuchukua hatua. Muda uliopangwa wa miaka 15 ya SDGs na miaka kumi ya mwanzo ya utekelezaji wa mpango wa Ajenda 2063 unawakilisha mipango ya muda inayowezekana ambayo kwayo serikali za Kiafrika tayari zimeahidi kutekeleza zenyewe.

Serikali za Kiafrika hazina budi kuondosha mapokeo ya kijamii yenye madhara na vikwazo vya kimila ambavyo vina athari mbaya kwa wanawake na familia zao.

Nyongeza Faharisi ya Maendeleo ya Watu Afrika (HDI) nafasi, thamani na mienendo

		Thamani ya Faharisi ya Maendeleo ya Watu (HDI)							Nafasi katika HDI			Wastani wa ukuaji (%) wa HDI kwa mwakaa		
Maendeleo ya Juu	Nchi									Badiliko				
		1990	2000	2010	2011	2012	2013	2014	2013	2009-2014	1990-2000	2000-2010	2010-2014	1990-2014
Maendeleo ya Juu Sana ya Watu														
Maendeleo ya Juu ya Watu														
63	Mauritius	0.619	0.674	0.756	0.762	0.772	0.775	0.777	62	6	0.86	1.15	0.68	0.95
64	Seychelles	–	0.715	0.743	0.752	0.761	0.767	0.772	68	8	–	0.39	0.97	–
83	Algeria	0.574	0.640	0.725	0.730	0.732	0.734	0.736	84	4	1.09	1.26	0.35	1.04
94	Libya	0.679	0.731	0.756	0.711	0.745	0.738	0.724	83	-27	0.75	0.34	-1.07	0.27
96	Tunisia	0.567	0.654	0.714	0.715	0.719	0.720	0.721	96	-1	1.43	0.88	0.26	1.00
Wastani wa kundi		0.610	0.683	0.739	0.734	0.746	0.747	0.746	79		1.03	0.80	0.24	0.82
Maendeleo ya Watu ya Kiwango cha Chini														
106	Botswana	0.584	0.561	0.681	0.688	0.691	0.696	0.698	106	1	-0.41	1.96	0.61	0.74
108	Egypt	0.546	0.622	0.681	0.682	0.688	0.689	0.690	108	-3	1.31	0.90	0.33	0.98
110	Gabon	0.620	0.632	0.663	0.668	0.673	0.679	0.684	111	1	0.20	0.48	0.76	0.41
116	South Africa	0.621	0.632	0.643	0.651	0.659	0.663	0.666	117	4	0.17	0.18	0.87	0.29
122	Cabo Verde	–	0.572	0.629	0.637	0.639	0.643	0.646	122	2	–	0.96	0.66	–
126	Morocco	0.457	0.528	0.611	0.621	0.623	0.626	0.628	126	5	1.44	1.48	0.69	1.33
126	Namibia	0.578	0.556	0.610	0.616	0.620	0.625	0.628	128	3	-0.39	0.94	0.70	0.35
136	Rep. of the Congo	0.534	0.489	0.554	0.560	0.575	0.582	0.591	138	2	-0.87	1.25	1.61	0.42
138	Equatorial Guinea	–	0.526	0.591	0.590	0.584	0.584	0.587	137	-5	–	1.18	-0.18	–
139	Zambia	0.403	0.433	0.555	0.565	0.576	0.580	0.586	139	1	0.71	2.52	1.36	1.57
140	Ghana	0.456	0.485	0.554	0.566	0.572	0.577	0.579	140	-2	0.63	1.33	1.13	1.00
143	Sao Tome and Principe	0.455	0.491	0.544	0.548	0.552	0.553	0.555	143	-2	0.76	1.02	0.52	0.83
Wastani wa kundi		0.525	0.544	0.610	0.616	0.621	0.625	0.628	126	1	0.36	1.18	0.76	0.79
Maendeleo ya Watu ya Kiwango cha Chini														
145	Kenya	0.473	0.447	0.529	0.535	0.539	0.544	0.548	145	0	-0.58	1.70	0.92	0.62
149	Angola	–	0.390	0.509	0.521	0.524	0.530	0.532	149	1	–	2.70	1.11	–
150	Swaziland	0.536	0.496	0.525	0.528	0.529	0.530	0.531	149	-5	-0.78	0.57	0.28	-0.04
151	Tanzania (United Republic of)	0.369	0.392	0.500	0.506	0.510	0.516	0.521	151	2	0.60	2.46	1.05	1.44
152	Nigeria	..	..	0.493	0.499	0.505	0.510	0.514	152	2	–	–	1.06	–
153	Cameroon	0.443	0.437	0.486	0.496	0.501	0.507	0.512	154	6	-0.13	1.07	1.32	0.61
154	Madagascar	–	0.456	0.504	0.505	0.507	0.508	0.510	153	-4	–	1.02	0.27	–
155	Zimbabwe	0.499	0.428	0.461	0.474	0.491	0.501	0.509	158	12	-1.53	0.75	2.50	0.08
156	Mauritania	0.373	0.442	0.488	0.489	0.498	0.504	0.506	156	1	1.71	0.98	0.92	1.28
159	Comoros	..	..	0.488	0.493	0.499	0.501	0.503	158	-1	–	–	0.75	–
161	Lesotho	0.493	0.443	0.472	0.480	0.484	0.494	0.497	161	1	-1.05	0.62	1.30	0.03
162	Togo	0.404	0.426	0.459	0.468	0.470	0.473	0.484	167	3	0.52	0.76	1.29	0.75
163	Rwanda	0.244	0.333	0.453	0.464	0.476	0.479	0.483	163	5	3.16	3.13	1.61	2.89
163	Uganda	0.308	0.393	0.473	0.473	0.476	0.478	0.483	164	-2	2.47	1.86	0.51	1.89
166	Benin	0.344	0.392	0.468	0.473	0.475	0.477	0.480	165	-2	1.33	1.78	0.64	1.40
167	Sudan	0.331	0.400	0.465	0.466	0.476	0.477	0.479	165	-5	1.90	1.52	0.74	1.55
168	Djibouti	–	0.365	0.453	0.462	0.465	0.468	0.470	168	0	–	2.17	0.97	–
169	South Sudan	–	..	0.470	0.458	0.457	0.461	0.467	171	..	–	–	-0.15	–
170	Senegal	0.367	0.380	0.456	0.458	0.461	0.463	0.466	170	-3	0.36	1.83	0.55	1.00
172	Côte d'Ivoire	0.389	0.398	0.444	0.445	0.452	0.458	0.462	172	0	0.23	1.12	0.98	0.72
173	Malawi	0.284	0.340	0.420	0.429	0.433	0.439	0.445	174	2	1.83	2.14	1.49	1.90
174	Ethiopia	–	0.284	0.412	0.423	0.429	0.436	0.442	175	2	–	3.78	1.78	..
175	The Gambia	0.330	0.384	0.441	0.437	0.440	0.442	0.441	173	-2	1.55	1.38	-0.02	1.22
176	Dem. Rep. of the Congo	0.355	0.329	0.408	0.418	0.423	0.430	0.433	176	3	-0.77	2.18	1.52	0.83
177	Liberia	–	0.359	0.405	0.414	0.419	0.424	0.430	177	1	–	1.20	1.50	–
178	Guinea-Bissau	–	..	0.413	0.417	0.417	0.418	0.420	178	-4	–	–	0.42	–
179	Mali	0.233	0.313	0.409	0.415	0.414	0.416	0.419	179	-3	2.97	2.73	0.61	2.47
180	Mozambique	0.218	0.300	0.401	0.405	0.408	0.413	0.416	180	0	3.25	2.96	0.94	2.74
181	Sierra Leone	0.262	0.299	0.388	0.394	0.397	0.408	0.413	182	0	1.32	2.63	1.59	1.91
182	Guinea	–	0.323	0.388	0.399	0.409	0.411	0.411	181	1	–	1.83	1.50	–
183	Burkina Faso	–	–	0.378	0.385	0.393	0.396	0.402	184	2	–	..	1.58	–
184	Burundi	0.295	0.301	0.390	0.392	0.395	0.397	0.400	183	0	0.20	2.62	0.66	1.28
185	Chad	–	0.332	0.371	0.382	0.386	0.388	0.392	186	1	–	1.12	1.37	–
186	Eritrea	–	–	0.381	0.386	0.390	0.390	0.391	185	-5	–	–	0.62	–
187	Central African Republic	0.314	0.310	0.362	0.368	0.373	0.348	0.350	187	0	-0.14	1.58	-0.84	0.45
188	Niger	0.214	0.257	0.326	0.333	0.342	0.345	0.348	188	0	1.85	2.40	1.69	2.05
Maendeleo ya Watu ya Kiwango cha Chini		0.351	0.372	0.441	0.447	0.452	0.455	0.459	169	0	0.88	1.82	0.97	1.26

Chazo: Imeandaliwa na Timu ya AfHDR kutoka UNDP (2015).

MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU
GOALS
1 HAKUNA UMASKINI
2 HAKUNA NJAA
3 AFYA NJEMA NA USTAWI
4 ELIMU BORA
5 USAWA WA JINSIA
6 MAJI SAFI NA USAFI
7 NISHATI NAFUU NA NISHATI MBADALA
8 KAZI YENYE HADHI NA UKUAJI UCHUMI
9 VIWANDA, UBUNIFU NA MIUNDOMBINU
10 KUPUNGUZA UKOSEFU WA USAWA
11 MIJI NA JAMII ENDELEVU
12 MATUMIZI NA UZALISHAJI KWA KUWAJIBIKA
13 KUCHUKUA HATUA JUU YA HALI YA HEWA
14 UHAI KWENYE MAJI
15 UHAI JUU YA ARDHI
16 AMANI, HAKI NA TAASISI MADHUBUTI
17 USHIRIKA KUFIKIA MALENGO
MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU
GOALS

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
Ofisi ya Kanda ya Afrika
One United Nations Plaza
New York, NY 10017

Empowered lives.
Resilient nations.

www.undp.org

Katika muktadha wa dunia inayobadilika, Ajenda ya Maendeleo ya 2030, na ukweli kwamba wanawake wanaunda nusu ya idadi ya watu, shauku ya maendeleo ya bara kama inavyofafanuliwa katika Ajenda 2063 haitafikiwa ikiwa nusu ya watu wataachwa nyuma. Ripoti ya Maendeleo ya Watu Afrika ya 2016 inachota kutoka katika mtazamo huu na kutoa mchango mzito katika mjadala wa maendeleo kuhusu usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake barani Afrika.

Ripoti hii ni ushahidi shadidi kwamba usawa wa jinsia ni kiwezeshi muhimu cha maendeleo yote. Kama maendeleo hayagusi jinsia basi yatahatarishwa. Kuchukua mkabala wa kupendeza wa uchumi-siasa kwa kuchimbua mapokeo ya kijamii, taratibu za jadi na miundo ya kitaasisi ambayo ina athari katika usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake, ripoti inachambua michakato ya kisiasa, uchumi na kijamii ambayo itakwamisha maendeleo ya wanawake wa Kiafrika na inapendekeza mikakati, sera na hatua madhubuti za kuchukua.

Kadiri wanawake wa Kiafrika wanavyopata mafanikio ya kiuchumi na kijamii, ndivyo jamii nzima inavyonufaika. Hatua kubwa zimepigwa katika kuimarisha ushiriki wa wanawake wa Kiafrika katika masuala ya kiuchumi na kisiasa. Hata hivyo, kasi ya kuharakisha usawa wa jinsia imekuwa chini kuliko ilivyotarajiwa na imekosa mwelekeo madhubuti kuliko inavyotamaniwa kwa kuwa kumekuwa na maendeleo duni katika kushughulikia mapokeo ya kijamii na taasisi ambazo zinaendeleza ukosefu wa usawa wa jinsia.

Matokeo yake, wanawake wengi wa Kiafrika wanabaki wamekwama katika uwanda wa chini wa fursa za kiuchumi, wakiendelea kushikilia hali ileile ya kiuchumi kwa ajili ya familia zao. Leo, wanawake wa Kiafrika wanapata tu asilimia 87 ya matokeo ya maendeleo ya watu kulinganisha na wanaume. Ukosefu wa usawa wa jinsia katika soko la kazi peke yake kuliigharimu Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kiasi cha Dola za Marekani Bilioni 105 kwa mwaka 2014—sawa na asilimia 6 ya Pato Ghafi la Taifa (GDP).

Kwa kutazama tofauti hizo kubwa za kijinsia, kufikia malengo ya SGD na Ajenda ya Afrika ya 2063 itakuwa tu ni kihamasisho, na si hali halisi. Ripoti hii inapendekeza Ajenda ya Kuchukua Hatua kwa mikakati saba ya utekelezaji ili kuharakisha usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake:

- Kupitisha mageuzi yenye tija ya kisheria na kisera kwa ajili ya uwezeshaji wanawake na kutumia usawa wa jinsia kama lensi ya kuongozea sera kwa ajili ya uwekaji mipango yote ya maendeleo na utekelezaji;
- Kujenga uwezo na uwajibikaji ili kukuza ushiriki wa wanawake na uwongo katika kutoa uamuzi katika ngazi zote za jamii;
- Kushughulikia vyanzo vya vitendo vya ubaguzi katika afya na elimu, kuondoa mapokeo ya kijamii na vikwazo vya kijadi vyenye kuumiza ambavyo vinazuia uletaji wa usawa wa jinsia;
- Kusaidia upataji kwa usawa wa ardhi, huduma za fedha, malipo sawa na ajira sawa kwa wanawake wa Kiafrika ikiwemo kuanzishwa kwa Benki ya Uwekezaji ya Wanawake Afrika na kufungua Fursa za Uwekezaji katika Benki za Maendeleo;
- Kuchukua uamuzi wa kimkakati na uwekezaji ili kuunda taasisi zenye uwezo zaidi, zinazotoa majibu kwa jamii, zenye uwakilishi kwa usawa na yenye kufanya mambo kwa haraka ambazo zitasaidia kutengeneza jamii iliyo na usawa na jumuishi zaidi;
- Kufuatilia uchambuzi unaoshughulikia masuala ya jinsia kikamilifu na kusimamia maendeleo na pia kusambaza zaidi maarifa, zana na uzoefu katika nchi na kanda mbalimbali; na
- Kuunda umoja wenye nguvu zaidi miongoni mwa makundi ya jamii katika kuelekea ajenda za pamoja kwa ajili ya uchukuaji hatua na kuharakisha usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake katika Afrika ikiwemo ahadi ya taasisi za umma na sekta ya binafsi, asasi za kiraia katika mradi wa Ithibati ya Usawa wa Jinsia kwa Afrika.

"Hii siyo hiyari, bali ni lazima: kushindwa kushughulikia ukosefu wa usawa wa jinsia na ubaguzi dhidi ya wanawake kutafanya iwe vigumu kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu" – Mtawala wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Helen Clark

"Kuamsha ile nguvu ya ubunifu ya wanawake, kwa kulea matamanio yao, kuhamasisha kupata kwao fursa na rasilimali na kuwapa nafasi ya kuwa raia wenye mchango kutachangia katika kuifanya Afrika iwe kinara wa karne ya 21 katika maendeleo jumuishi" – Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa Abdoulaye Mar Dieye.

"Historia itatuhukumu si kwa yale tunayosema katika wakati huu, bali kwa yale tutakayofanya ili kuinua maisha ya raia wenzetu waume kwa wake. Itatuhukumu kwa kumbukumbu tunazowaachia vizazi vijavyo" – Rais wa Liberia, Ellen Sirleaf Johnson

"Suala muhimu katika maendeleo ya Afrika, amani na ustawi ni ushiriki wa wanawake wake, hasa uwezeshaji wao kiuchumi. Mkazo kwa mwanamke ni zaidi ya utegemezi kwa kijadi kwa wanaume, ni kutumia siyo nusu bali vipawa vyetu vyote kamilifu" Rais wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Nkosazana Dhlamini-Zuma

"Hakuna kupumzika hadi hapo dunia yetu ipate ukamilifu na uwiano unaostahili, ambapo wanaume na wanawake wanachukuliwa kuwa sawa na huru" Leymah Gbowee, Msindi wa Nishani ya Nobeli ya Amani

"Mbegu za mafanikio katika kila taifa duniani zinakuwa bora zaidi zinapopandwa na wanawake na watoto" Rais wa zamani wa Malawi Joyce Banda

"Afrika imepiga hatua kubwa katika malengo yake yaliyo mengi ya maendeleo lakini mambo zaidi hayana budi kufanywa katika kukabili ukosefu wa usawa katika aina zake zote, kwa kutumia usawa wa jinsia kama kiongeza kasi cha kupata Malengo yote ya Maendeleo Endelevu" Mchumi Mkuu wa Afrika, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Ayodele Odusola